# Je, madhara gani yatawapata wasichana na wavulana wanaojamiiana kwa kutumia sehemu ya haja kubwa?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Tunasema ngono kutumia njia ya haja kubwa pale ambapo uume uliodinda unaingizwa kwenye njia ya haja kubwa (mkunduni).

Tatizo kubwa la kujamii ana sehemu ya haja kubwa, ni kwamba kuna uwezekano wa kueneza magonjwa ya zinaa pamoja na maambukizi ya VVU na UKIMWI zaidi kuliko kutumia njia ya kawaida ya uke. Kujamii ana sehemu ya haja kubwa ni hatari kwa sababu hakuna yale majimaji kama ukeni na ngozi ni laini sana. Kwa hiyo michubuko i inaweza kutokea kwa urahisi. Michubuko hii i ii inasababisha maumivu na pia i inarahisisha kuambukizana magonjwa ya zinaa. Kama bado umeamua kujamii ana kwa kutumia njia ya haja kubwa pamoja na usumbufu wote tulioutaja hapo juu, unashauriwa kutumia kondomu i li kuzuia uambukizaji wa magonjwa.